

FASIHI SIMULIZI MODELI 2562021602

 atikaschool.org/kcse-kiswahili-fasihi/fasihi-simulizi-modeli-2562021602

FASIHI SIMULIZI

- a) Fafanua mchakato/fomula ya uwasilishaji wa vitendawili. (alama4)
- b) Linganisha naulinganue vitendawili na methali.. (alama10)
- c) Toa sababu sita za kudidimia kwa fasihi simulizi. (alama6)

MWONGOZO

FASIHI SIMULIZI

- **a) Fafanua mchakato wa uwasilishaji wa vitendawili. (al.4)**
 - 1. Kitangulizi- Mtegaji: kitendawili
Mteguaji: tega
 - 2. Swali lenyewe- kitendawili kutegwa
 - 3. Majibu kutolewa
 - 4. Mtegaji asipooridhika huomba kupewa zawadi kisha hutoa jibu.
- **b) Linganisha na ulinganue vitendawili na methali. (al.10)**

Mfanano

 - 1. Zote ni tungo fupi za semi
 - 2. Zote huwa na maana fiche
 - 3. Zote hutumia lugha inayojenga taswira
 - 4. Zote huwa na miundo maalum ya lugha
 - 5. Zote hupata maana kulingana na jamii
- **Tofauti**
 - 1. Vitendawili vina fomula ilhali methali hazina fomula
 - 2. Fumbo la kitendawili hufumbuliwa papo hapo fumbo si lazima kufumbuliwa papo katika methali.
 - 3. Vitendawili hutumiwa na watoto sana, methali hutumiwa kuonyesha hekima miongoni mwa watu wazima na wazee
 - 4. Vitendawili hutolewa katika vikao maalum, methali si lazima kutengewa vikao maalum.
 - 5. Vitendawili hutumia lugha ya majibizano , methali aghalabu huwa kauli moja ya msemaji.
 - 6. Hadhira tendi huwa katika vitendawili , katika methali hadhira si lazima iwe tendi.

- **C) Uhamaji wa watu huwafanya kuacha utamaduni wao.**
 - watu kuwa na mtazamo hasi kuhusu fasihi simulizi
 - ubidhaaishaji wa fasihi simulizi- kuandika kitabu kama vile cha methali na kubadilisha umiliki
 - watu kupendelea kusoma
 - mwingiliano wa watu huwafanya kusahau fasihi yao
 - teknolojia yasasa ambayo fasihi simulizi huhifadhiwa badala yaakilini.
 - Utamaduni wa fasihi simulizi umebadilika – babu na bibi hawawatambii watoto hadithi. Mwalimu akadirie